BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA JUU YA UWASILISHWAJI WA TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika;** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba mbingu na ardhi, kwa kutujaalia afya njema, taufiki na kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwa ajili ya kuendeleza majukumu yetu muhimu ya kuishauri Serikali pamoja na kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo hiki muhimu cha kitaifa.

**Mheshimiwa Spika;** aidha, natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya uwasilishwaji wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** vile vile, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Taarifa ya Hali ya Dawa za kulevya kwa mwaka 2022 na 2023, ikiwa ni miaka miwili toka kuanza utekelezaji wa Sheria mpya iliyoanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar Sheria Nam. 8 ya mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika;** kipekee, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi

Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa yanayoendelea katika Kamati hii yenye kuonesha ufanisi mkubwa katika kutimiza wajibu wao ndani ya chombo hiki kitukufu katika nchi yetu ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe.Maryam Thani Juma - M/Mwenyekiti
3. Mhe.Abdalla Abass Wadi - Mjumbe
4. Mhe.Mussa Foum Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Haji Shaaban Waziri - Mjumbe
6. Mhe: Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
7. Mhe.Panya Ali Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Mjumbe
9. Ndugu Ali Alawy Ali - Katibu
10. Ndugu Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu
11. Ndugu Shawana Mohammed Haji - Katibu
12. Ndugu Amina Abeid Hemed - Mkalimani

**Mheshimiwa Spika;** kadhalika, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Unguja na Pemba wakiongozwa na

Kamishna Mkuu Kanal Burhan Zuberi Nassor kwa namna wanavyoweza kuendeleza juhudi za kudhibiti Usafirishaji, Usambazaji na Utumiaji wa Dawa za kulevya nchini. Ni jambo la faraja kuona hadi sasa Zanzibar imebainika haizalishi dawa za kulevya isipokua imethibitika kwamba Dawa zote zinazokamatwa katika maeneo yote ya visiwa hivi zinatoka nje ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** wakati Kamati ikipitia taarifa hii imepata wasiwasi mkubwa kuona kwamba kuna ongezeko kubwa la matumizi ya dawa za kulevya yanayoendelea kuripotiwa na Shirika la UNODC ambayo husababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji na jamii ambayo huchangia ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa ya afya ya akili na homa ya ini B na C. Hivyo, kamati inaishauri Mamlaka kujenga mashirikiano na Tume ya Ukimwi na Wizara ya Afya ili kuhakikisha kwa pamoja wanapiga vita maambukizi ya maradhi haya kwa waathirika wa dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika;** kwa mujibu wa taarifa hii nchi za Mashariki ya Kati na Kusini Magharibi mwa Asia, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya dawa zenye tiba asili ya kulevya zinazotumika kutibu maradhi mbali mbali, bila kufuata ushauri wa daktari. Kamati inashauri Serikali kuongeza ushirikiano na vyombo vya udhibiti vya Ulinzi na Usalama, UK border force, FIU na wananchi kwa ujumla ili kuhakikisha dawa hizi hazifiki nchini kwa namna yoyote ile ikiwemo matumizi ya tiba ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika;** sambamba na hili Kamati inaiomba Serikali kuweka ulinzi wa kutosha kwenye njia za bandari kuu, bandari bubu na viwanja vya ndege ili kuondosha mianya ya uingizwaji wa dawa mpya za kulevya NPS zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali ziliopo kwenye dawa za

kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama vile bangi, heroin, mirungi na kokeni zinazosababisha tatizo la kiafya na kuongeza tishio la usalama kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika;** vilevile, Kamati inapenda kutoa tahadhari juu ya dawa zenye asili ya Tramadol kuweka udhibiti wa matumizi ya dawa hizo baada ya kubainika kuwa na madhara katika afya ya mwanadamu endapo zitatumika zaidi ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika;** katika sura ya Nne inayozungumzia Kupunguza uhitaji wa Matumizi ya Dawa za Kulevya. Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kushirikiana na wadau kwenye utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari, vyombo vya ulinzi na usalama, machapisho na maadhimisho mbali mbali ya kitaifa. Ili jamii isijihusishe na matumizi ya dawa hizo, kamati inasisitiza elimu zaidi iendelee kutolewa kwa vijana wetu kupitia sehemu za mikusanyiko na shughuli za kijamii juu ya madhara yanayopatikana kupitia matumizi ya dawa haramu za kulevya.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati inatoa pongezi kwa Mamlaka kuweza kuanzisha Tiba kwa Waraibu wa Dawa za kulevya na Marekebisho ya Tabia katika kituo kilichopo Kidimni. Ni jambo la kuridhisha kuona hadi tunapitia taarifa hii, jumla ya waraibu 300 walipokelewa na kunufaika na tiba hiyo. Aidha, kutokana na Serikali kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19 imeendelea kufadhili mafunzo ya stadi za kazi kwa waraibu wanaopata nafuu katika kituo hicho. Kamati inasisitiza Serikali kuendeleza mafunzo ya kazi za mikono ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea wanapomaliza huduma ya matibabu sambamba na kuanzisha kituo kama hichi kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** kamati imefarijika sana kuona Mamlaka imekamata jumla ya kesi 498 za watuhumiwa wa dawa za kulevya na kufanikiwa kutia hatiani kesi 26 zenye watuhumiwa 27 ambazo Mahakama imewapa adhabu mbali mbali hadi kutumikia kifungo cha maisha. Hata hivyo, inashauriwa wananchi wasichoke kwenda kutoa ushahidi wa mashauri yanayohusiana na dawa za kulevya Mahakamani kila wanapohitajika, kufanya hivyo kutasaidia watuhumiwa wengi kuwatia hatiani na kupunguza tatizo hili kuendelea.

**Mheshimiwa Spika;** kadhalika, Kamati inawaomba wananchi kuendeleza masharikiano ya mapambano dhidi ya uhalifu wa dawa za kulevya kwa kuitumia huduma ya mawasiliano ya simu ya utoaji taarifa zinazohusu biashara hii haramu kwa namba **0774 - 33 33 00** ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa pamoja na kuwataka wanajamii kuachana na muhali ambao utawarudisha nyuma kufichua na kutoa taarifa za wahalifu.

**Mheshimiwa Spika;** mwisho kabisa, napenda niseme kuwa mapambano ya udhibiti wa matumizi, uuzaji na uingizaji wa dawa za kulevya ubaki historia ni vyema Serikali ikazifanyia kazi changamoto kuu za Mamlaka ikiwemo ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kiuchunguzi na vifaa vya kufanyia operesheni, kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sheria Nam. 8 ya 2021 kwa vifungu vinavyosababisha watuhumiwa kuachiwa huru, kutofanyiwa taratibu za kutaifisha vyombo vinavyokamata na dawa na kutiliwa fedha za kutosha za uwendeshaji wa Mamlaka. kufanya hivyo, kutasaidia Mamlaka kufanya kazi kwa weledi na ustadi mkubwa na lengo la Zanzibar bila dawa za kulevya litapatikana.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kumalizia, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii ya maoni ya maoni ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika;** **Naomba Kuwasilisha.**

..................................

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za**

**Viongozi Wakuu wa Kitaifa**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**